



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

*Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:*

**Tel:** +255 659 566703 (Direct line)

S.L.P. 70, SIKONGE

**Fax:**

**TABORA**

**e-mail:** [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)

**Unapojibu tafadhali taja :**

Kumb. Na. HWS/M.30/44/10

**Tarehe: 25/02/2021**

## **TANGAZO LA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge anawatangazia wananchi wote wa Wilaya ya Sikonge kuomba nafasi ya kazi zifuatazo: -

### **1. AFISA NYUKI II / AFISA NYUKI MSAIDIZI II (Nafasi 1)**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- (iii) Awe na elimu ya kidato cha nne, shahada/stashahada ya fani ya nyuki.
- (iv) Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu (3).

#### **MASHARTI YA AJIRA**

- Ajira hii ni ya mkataba.

#### **MSHAHARA**

Kulingana na kiwango cha taaluma mshahara atalipwa **Tsh 300,000/=** au **500,000/=** kwa mwezi kulingana na kiwango cha taaluma.

### **2. WAKUSANYA MAPATO (REVENUE COLLECTOR) (Nafasi 8)**

#### **SIFA ZA MWOMBAJI**

- (iv) Awe na umri kati ya miaka 18 hadi miaka 45.
- (v) Awe ni mkazi wa sikonge.
- (vi) Awe amehitimu mafunzo angalau ya cheti katika fani ya uhasibu /fedha/ugavi.

#### **MASHARTI YA AJIRA**

- Ajira hii ni ya mkataba.

#### **MSHAHARA**

Asilimia (10%) ya makusanyo yanayowasilishwa kwa kila mwezi.

### 3. AFISA HABARI NA MAWASILIANO (Nafasi 1)

#### SIFA ZA MWOMBAJI

- (iv) Awe na umri kati ya miaka 18 hadi miaka 45.
- (v) Awe ni mkazi wa sikonge.
- (vi) Awe na elimu ya kidato cha nne, shahada/stashahada ya fani ya Uwandishi wa Habari.

#### MASHARTI YA AJIRA

- Ajira hii ni ya mkataba.

#### MSHAHARA

Kulingana na kiwango cha taaluma mshahara atalipwa **Tsh 500,000/=** au **300,000/=** kwa mwezi kulingana na kiwango cha taaluma.

#### MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA WAOMBAJI WOTE

- Maombi yaambatanishwe na vivuli vya vyeti, picha moja ya passport size iliyopigwa hivi karibuni, maelezo binafsi (CV) ya mwombaji na namba ya simu.
- Mwombaji aambatanishe kwenye maombi ya kazi nakala za barua za wadhamini wawili wanaofahamika katika jamii.
- Maombi yote yawasilishwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),  
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge,  
S.L.P 70

**SIKONGE.**

**Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 12/03/2021 saa 9.30 mchana.**

<sup>TEL</sup>  
Tito E. Luchagula  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**SIKONGE.**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**WILAYA - SIKONGE.**